
BUSATI MICHEZO
FADLU AIPA RAHA SIMBA

busati @busati @busati

# BUSATI

Twende Pamoja

Tovuti: www.busati.co.tz | ISSN 3590-6236 Toleo Na.11 Busati Jumanne Januari 28, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100

## Mkutano M300...

# Rais Samia kuipa neno Afrika



- Asubiriwa ili atoe jambo la matumaini kwa kina mama afrika
- Ndiye mbeba ajenda ya nishati safi

HABARI UK. 2




# Biteko ataja upatikanaji wa nishati afrika

# Watanzania wengi sasa wanufaika

NA MWANDISHI MAALUM

RAIS Dkt. Samia Suluhu Hassan amewezesha mabilioni ya mikopo kwa wanufaika zaidi ya milioni 1.7 ambao wapo katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwasaidia kujikwamua kutoka pale walipo.

Dkt. Samia pia amefanikiwa kutoa mikopo isiyo na riba ya Sh bilioni 240.9 kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu na kutoa elimu

Inaendela -Uk. 3



# Utalii unavyozidi kupaa nchini

NA MWANDISHI WETU

WAKATI Tanzania ikivutia wengi kwa sasa, huku ikitajwa ni sehemu bora zaidi ya kutembelea kwa mwaka 2025, yote hayo ni maono ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuipambania sekta hiyo.

Inaendela -Uk. 3



# RAIS SAMIA KUIPA NENO AFRIKA

NA MWANDISHI WETU

WAKATI Mkutano wa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika ujulikanao kama Mission 300, ukiwa umeanza jana, Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa 'kuishusha pumzi' Afrika pale atakapounguruma kwenye mkutano huo leo

Rais Dkt. Samia ambaye amejitwisha zigo la kuipigania nishati safi, anatarajiwa kusikilizwa na wengi haswa kina mama wa Afrika, ambao wengi wana matarajio makubwa naye ya kuwasemea juu ya adha wanazopata kutokana na ukosefu wa nishati safi.

Akiwa ameibeba ajenda ya nishati salama mkononi mwake, Rais Dk. Samia amevunja na kuandika rekodi ya aina yake kwa kuwa Rais wa kwanza nchini aliyewahi kupokea idadi kubwa ya wakuu wa nchi 25 kujai kwa pamoja nchini.

Nchi ambao wakuu wake wamethibitisha kushiriki ni Algeria, Comoro, Liberia, Lesotho, Botswana, Kenya, Ghana, Gabon, Sierra Leone, Ethiopia, Sudan, Malawi, Zambia, Somalia, Guine Bisau, Burundi, Mauritania, Kongo Brazzaville, Madagascar, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Libya, Nigeria, Djibouti na Gabon.

Wakati akizungumzia kwa kina mkutano huo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt.Doto Biteko alisema, utakuwa ni fursa kubwa sana kwa Watanzania.

"Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana ya kuitangaza Tanzania kimataifa, hii imepeleka taasisi za kimataifa, kampuni na wawekezaji kuona Tanzania kuwa ni sehemu sahihi ya kufanya biashara na uwekezaji na mfano halisi ni Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo Afrika kuichagua Tanzania kufanya mkutano huu mkubwa wa kimataifa utakahudhuriwa viongozi kitoka nchi 54 barani Afrika." Amesema Dkt. Biteko

Ameongeza kuwa, sababu nyingine kubwa ya Tanzania kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa Mkutano huo ni mafanikio yaliyofikiwa katika sekta ya nishati ikiwa ni pamoja na kupeleka umeme kwa wananchi suala linaloendanana Ajenda ya mkutano huo ya kuharakisha kupeleka umeme kwa wananchi milioni 300 barani Afrika ifikapo 2030 kati ya watu milioni 685 ambao bado hawana umeme.

"Taifa limepiga hatua kubwa katika Sekta ya Nishati, tunamshukuru Rais kwa msukumo mkubwa anaotoa katika Sekta ya Nishati, taifa lina umeme wa kutosha na wa ziada, uzalishaji sasa umepanda kutoka megawati 1470 hadi megawati takriban 3,077."

Amesema upatikanaji wa umeme barani Afrika kwa sehemu kubwa uko chini ya asilimia 50 lakini Tanzania imepiga hatua kubwana ipo kwenye asilimia zaidi ya 78.

Akiongeza kuhusu mafanikio ya Sekta ya Nishati, Dkt. Biteko amesema vijiji vyote 12,318 Tanzania sasa vimesambaziwa umeme na tathmini iliyofanywa na Benki ya Dunia barani Afrika mwaka jana imeonesha kuwa Tanzania iliongoza kwa kusambazia wananchi umeme vijijini .

Dkt. Biteko ameeleza kuwa, baada ya umeme kufika kwenye vijiji vyote sasa kasi inaelekea kwenye vitongoji ambapo katika vitongoji 64,000 nchini, vitongoji takriban 36,000 vimepelekewa umeme.

Ametaja faida za mkutano wa M300 kwa Tanzania kuwa ni pamoja na kuongeza fursa za kupata fedha za kuendelea miradi mbalimbali, kuongeza fursa za uwekezaji, kupata uzoefu kutoka kwa waliofanikiwa zaidi kwenye sekta ya nishati na kuongeza heshima ya nchi kimataifa.

Ameongeza kuwa faida nyingine ni kuharakisha upatikanaji umeme nchini ambapo kiasi cha wananchi watakaounganishiwa umeme kupitia M300 ni milioni 8.3 ifikapo 2030 na hivyo kuifanya Tanzania kuunganisha wateja milioni 13.5 kufikia 2030 Kutoka milioni 5.2 ya sasa.

## BITEKO ATAJA UPATIKANAJI WA NISHATI AFRIKA




NA MWANDISHI WETU

NCHI za Afrika zimeelezwa kupiga hatua katika suala zima la upatikanaji nishati ya umeme toka nyingi kati ya hizo zipte uhuru miaka ya 1960.

Akisema hilo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amesema baada ya kupata uhuru, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao.

Dk. Biteko alisema hayo jana kwenye Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika 'Mission 300' unaofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es salaam

"Inasikitisha kwamba idadi ya Waafrika ambao hawana umeme inakadiriwa kuwa milioni 571. kutokana na hali hii, Mkutano huu uliitishwa, ukiwa na lengo kubwa lakini linaloweza kufikiwa la kuongeza upatikanaji wa umeme kwa angalau watu milioni 300 barani Afrika katika miaka mitano ijayo

"Kama ilivyobainishwa katika Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), leo Dar es Salaam inayo heshima ya kuwa mwenyeji wa wajumbe kutoka Afrika na kwingineko, wakihudhuria Mkutano huu muhimu unaolenga kuimarisha azma ya Afrika ya kuipatia bara hili nishati.

"Baada ya kupata Uhuru mwaka 1960, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao. Tanzania ilikuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 21 pekee wakati wa Uhuru, kwa sasa nchi ina uwezo wa kuzalisha megawati 3,160."

SOMA ZAIDI UK 8&9




# WATANZANIA WENGI SASA WANUFAIKA

NA MWANDISHI MAALUM

RAIS Dkt. Samia Suluhu Hassan amewezesha mabilioni ya mikopo kwa wanufaika zaidi ya milioni 1.7 ambao wapo katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwasaidia kujikwamua kutoka pale walipo.

Dkt. Samia pia amefanikiwa kutoa mikopo isiyo na riba ya Sh bilioni 240.9 kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu na kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana 164,443 waliomaliza taasisi za elimu ya juu na kati.

Pia kiwango cha ukuaji wa pato la taifa kimekuwa kutoka asilimia 4.8 mwaka 2020 hadi asilimia 5.1 mwaka 2023.

Hayo yamefichuliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, wakati anasoma utekelezaji wa Serikali wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mwaka 2020-2025 iliyowasilishwa katika Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM Taifa uliomalizika jijini Dodoma.

Majaliwa alimwaga data hizo na kusema, kiwango cha ukuaji wa uchumi kilikadiriwa kukua kwa asilimia 5.4 mwaka 2024 na kwamba serikali imedhibiti mfumuko wa bei hadi asilimia 3 mwaka 2024 kutoka asilimia 3.1 mwaka 2020.

"Serikali imetekeleza miradi 17,421 ya sekta za afya, elimu na maji na kutoa ajira za muda kwa kaya za walengwa 662,374 Tanzania Bara na Zanzibar, kutoa mikopo isiyo na riba ya Sh bilioni 240.9 kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu na kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana 164,443 waliomaliza taasisi za elimu ya juu na kati.

Majaliwa akimwaga data hizo alisema; "Mapato ya ndani yaliongezeka kufikia Sh trilioni 13.54 mwaka 2024 kutoka Sh trilioni 8.1 mwaka 2020. Idadi ya walipa kodi iliongezeka hadi milioni 6.4, na serikali imeondoa kodi zisizo na tija ili kuchochea maendeleo," alisema.

Katika kupambana na umaskini na kuwawezesha wananchi kiuchumi, Majaliwa alieleza serikali imeweza kutoa huduma za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa kaya 1,357,965 katika vijiji, mitaa na shehia 17,260 Tanzania Bara na Zanzibar.

Juu ya akiba ya fedha za kigeni, ilifikia Dola za Marekani bilioni 5.05, zikitosheleza uagizaji wa bidhaa kwa asilimia 4.1. Mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliongezeka kutoka Dola bilioni 8.81 mwaka 2020 hadi Dola bilioni 14.66 mwaka 2024.

"Wastani wa mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yameongezeka kutoka Sh trilioni 1.47 Novemba, 2020 hadi Sh trilioni 2.37 Novemba, 2024 na Mtaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) umekua kutoka Sh bilioni 60 mwaka 2020 hadi Sh bilioni 438 mwaka 2024.

Aidha, madeni yaliyohakikiwa ya Sh trilioni 3.47 yamelipwa kwa wakandarasi, watumishi, watoa huduma, wazabuni na madeni mengineyo ya kimkataba na mikopo Sh bilioni 693.9 ilitolewa na serikali kwa wanufaika zaidi ya milioni 1.7.

Alisema serikali imeimarisha mfumo wa stakabadhi ghalani, ambapo vyama vya ushirika vimeongezeka kutoka 2,150 mwaka 2020 hadi 4,060 mwaka 2024 na kuchangia mchakato wa kuanzisha Benki ya Ushirika ambayo iko katika hatua za mwisho, ikiwemo kufikia lengo la ukwasi wa Sh bilioni 50.

"Uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kutoka tani milioni 18.6 mwaka 2020 hadi tani milioni 22.8 mwaka 2024. Uzalishaji huo ulichagizwa na kuongezeka kwa upatikanaji wa mbolea kwa asilimia 107 kutoka tani 586,604 mwaka 2020 hadi tani 1,213,729 mwaka 2024," alieleza Majaliwa. kilimo, mifugo na uvuvi.

# UTALII UNAVYOZIDI KUPAA

NA MWANDISHI WETU

WAKATI Tanzania ikivutia wengi kwa sasa, huku ikitajwa ni sehemu bora zaidi ya kutembelea kwa mwaka 2025, yote hayo ni maono ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuipambania sekta hiyo.

Haya yamekuja, baada ya Tanzania kutangazwa ni nchi bora zaidi ya kutembelea barani Afrika kwa mwaka 2025, ambapo zote hizo ni jitihada kubwa za Dkt. Samia.

Kwa mujibu wa jarida la U.S. News, ushindi huu mkubwa unaonesha wazi matunda ya uongozi mahiri wa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Tangu aingie madarakani, amekuwa mstari wa mbele katika kuimarisha sekta ya utalii kama injini muhimu ya uchumi wa taifa.

Rais Dkt. Samia amejitolea kwa dhati kutangaza Tanzania kimataifa, jambo lililoonekana wazi kupitia filamu ya kihistoria 'The Royal Tour'.

Wakati maono ya Dkt. Samia yakifanya kazi, Wizara ya Maliasili na Utalii imetakiwa kushirikiana kwa ukaribu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kukuza soko la utalii nchini na kurahisisha utoaji wa huduma ya viza kwa watalii.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Timotheo Mnzava katika kikao kilichofanyika bungeni jijini Dodoma.

"Wizara ya Mambo ya Ndani, Uhamiaji na Wizara ya Maliasili na Utalii mshirikiane kuikuza Sekta ya Utalii, tunahitaji mfanye zaidi kuisaidia sekta hii na kama kuna changamoto mkazitatue," Mnzava amesisitiza.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dkt. Pindi Chana ameiahidi kamati hiyo kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii itahakikisha inafanya kazi kwa ukaribu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhakikisha soko la utalii linakua ili kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan za kukuza Sekta ya Utalii nchini.

"Tutahakikisha tunatambua masoko muhimu ya utalii na kuweka mikakati madhubuti ya kuvutia watalii kwa kushirikiana," Chana amesema.

# UTALII UNAPOKUZWA NA MATAMASHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii Balozi Dkt. Pindi Chana amezitaka halmashauri za wilaya zote nchini kuanzisha Matamasha ya Utalii na Uhifadhi huku akielekeza suala la kuwalinda wananchi dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu kuwa ajenda ya kudumu.

Dkt. Chana ametoa kauli hiyo wakati akimwakilisha Mhe. Waziri Mkuu kufungua rasmi msimu wa pili wa Tamasha la Utalii la Same, ambalo lilifanyika mwishoni mwa mwaka jana ambapo pia alitoa zawadi na tuzo kwa wadau mbalimbali kutambua mchango wao katika kufanikisha Tamasha hilo

“Wakati tunasherekea Tamasha la Pili la Utalii la Same ni lazima tuhakikishe tunawalinda wananchi kutokana na wanyama wakali wakati huo huo tunahifadhi rasilimali tulizopewa na Mwenyezi Mungu ili zitusaidie kutuletea watalii zaidi “ alifafanua Dkt. Chana.

Amesema wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI na wananchi itaendelea kuhifadhi rasilimali kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Aidha amefafanua kuwa usemi wa Kiswahili usemao “Tunza mazingira yakutunze” unadhihirisha kuwa mazingira yakitunzwa vizuri ikiwemo misitu na maliasili yatasaidia kujenga uchumi.

“Tukitunza mazingira tutapata mvua, tutapata maji, tutalima, tutapata vyakula na mazao ya biashara, hakutakuwa na njaa wala umaskini wa kipato na pia tutaishi kutokana na Kuvuta hewa safi.Usemi huo una mashiko ni vyema tukarithisha watoto wetu kuanzia wawapo shuleni ili waweze kutambua umuhimu wa kutunza mazingira”ameongeza Mhe. chana

Amesema ni muhimu klabu za mazingira zilizopo katika maeneo yetu kuendelea kuzisimamia ili zilete tija kwani kupitia klabu hizo wanafunzi watajifunza hifadhi ya mazingira, utalii na pia watajenga uelewa wa kutosha kutenda popote wawapo kwa falsafa ya “Jenga kesho iliyo bora (BBT)”.

Amepongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassani kwa kuandaa Filamu ya Tanzania the Royal Tour na Amazing Tanzania ambapo amesema kuanzishwa kwa Tamasha la Utalii la Same ni kufuata maono yake katika kutangaza utalii.

Akifafanua kuhusu faida ya Tamasha hilo amesema limesaidia kuwaletea wageni, pia kutoa elimu mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji kama misitu wa Chome.

Pia kuhusu kuboresha na Tamasha hilo, Dkt. Chana ametaka kuwepo na mikakati madhubuti ya kuendeleza Tamasha hilo kwa Halmashauri kutenga bajeti kuliko kuwaachia wadau wachache na uongozi wa Wilaya hiyo huku akisisitiza kuwa suala la uhifadhi na utalii lipo kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

“Ndugu zangu suala hili ni la msingi sana hata baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alisisitiza kuwa rasilimali hizi lazima zilindwe na ndiyo maana tuna Jeshi la Uhifadhi”amefafanua Waziri Chana

Ametoa wito kwa wananchi kushirikiana na Serikali kuwabaini watu waovu, wanaotaka kuhujumu rasilimali za watanzania. “Kuna changamoto za maingiliano tuliangalie ili wasilete madhara”.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Metheusela Ntonda amesisitiza kuendelea kufungamanisha Utalii na utamaduni kwenye matamasha hayo.





# Je, wajua? Ajabu mifumo ya ekolojia ya nchi kavu

KAMPENI ya Siku ya Mazingira Duniani mara nyingi inaangazia uboreshaji wa ardhi, kuenea kwa majangwa na kustahimili ukame.

Ukame na kuenea kwa majangwa kunatishia mifumo muhimu ya ekolojia katika sayari nzima, ikijumuisha mifumo ya ekolojia ya maji safi na udongo, viungo muhimu vinavyowezesha aina zote za maisha Duniani.

Hapa kuna mambo muhimu yanayofanya mifumo ya ekolojia ya nchi kavu na ardhi kuwa ya kipekee sana na, katika hali zingine, ya kutia moyo.

**UDONGO NA MAJI**

Takriban asilimia 60 ya viumbe vyote huishi kwenye udongo, na hivyo kufanya ardhi kuwa makao ya viumbe hai wengi duniani.

Udongo wenye rutuba huhifadhi kiasi kikubwa cha hewa ya ukaa, ambayo, ikiwa itaachiliwa, inaweza kusababisha ongezeko kubwa la joto duniani.

Asilimia 0.5 ya maji Duniani tu ni maji safi yanayoweza kutumika na kupatikana. Mabadiliko ya tabianchi yanaathiri vibaya usambasaji wake.

Katika kipindi cha miongo miwili iliyopita, hifadhi ya maji ardhini—ikiwa ni pamoja na unyevu wa udongo, theluji na barafu— imeshuka kwa kiwango cha sentimeta 1 kwa mwaka na kuwa na madhara makubwa kwa utoshelezaji wa maji na uzalishaji wa chakula.

**MAENEO YALIOKAUKA**

Maeneo yaliokauka - eneo ambalo linakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji—linakalia asilimia 41 ya ardhi duniani na asilimia 78 ya maeneo ya malisho.

Maeneo yaliokauka huzalisha asilimia 44 ya mazao ya mimea duniani, ni chanzo cha chakula kwa nusu ya mifugo duniani na kusaidia maisha na kipato cha zaidi ya watu bilioni 2.

Licha ya jina lake, nchi kavu ni makazi kwa zaidi ya robo ya misitu ya duniani, theluthi moja ya maeneo yabayoanuai duniani na ni maeneo muhimu kwa ndege wa kuhamahama.

**MAJANGWA**

Majangwa hukalia zaidi ya humusi ya ardhi Duniani na hupatikana katika kila bara. Sahara ni jangwa kubwa zaidi la joto duniani, lina ukubwa wa kilomita mraba milioni 9.4, takribani ukubwa wa Canada.

Licha ya sifa yake ya kutokuwa na uhai, Jangwa la Sahara ni makazi kwa spishi 500 za mimea, spishi 70 za mamalia, spishi 100 za reptilia, spishi 90 za ndege, na athropoda kadhaa, kama vile buibui na nge.

Majangwa mengi yanapanuka kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi lakini baadhi ya nchi zinapambana zikiwemo nchi 22 za Afrika zinazopakana na Jangwa la Sahara ambapo Ukuta Mkubwa wa Kijani unaolenga kurejesha hekta milioni 100 za ardhi kupitia mandhari ya kijani na inayozalisha mazao.

**MISITU**

Misitu hukalia asilimia 31 ya Dunia lakini haijasambazwa kwa njia sawa kwani zaidi ya nusu ya misitu ya dunia inapatikana katika nchi tano pekee: Brazili, Kanada, Uchina, Shirikisho la Urusi na Marekani.

**MISITU NI MAKAZI KWA ZAIDI** ya nusu ya spishi za juu za ardhi za wanyama, mimea na wadudu duniani.

Zaidi ya spishi 28,000 za mimea kwa sasa zimeripotiwa kutumiwa kama dawa na nyingi zinapatikana katika mifumo ya ekolojia ya misitu.

Vijidudu vya udongoni ni muhimu katika kuzalisha antibiotiki. Penicillin, kwa mfano, hutoka kwa kuvu wadogo wanaoishi kwenye udongo.

Kiumbe kikubwa zaidi duniani ni kuvu katika Milima ya Bluu ya Marekani. Inakalia takriban hekta 965 za ardhi, kuvu inaweza kuwa ya zamani kama miaka 8,650 hivi, hali inayoweza kuifanya kuwa kati ya viumbe hai vikongwe zaidi ulimwenguni.

**MAJI SAFI**

Maziwa, mito na ardhioevu hushikilia kati ya asilimia 20 hadi 30 duniani ya hewa ya ukaa licha ya kukalia asilimia kati ya 5 na 8 tu ya ardhi yake.

Mto Nile unachukuliwa kuwa njia ndefu zaidi ya maji duniani. Inaanzia Afrika Mashariki, inapita katika nchi 11 tofauti na ina urefu wa kilomita 6,695.

Takriban vipato bilioni 1.4 kote duniani vinategemea moja kwa moja uwepo wa maji safi, ikijumuisha kazi zinazohusiana na sekta za chakula na vinywaji, nishati na maji.

**MASHAMBA**

Kila sekunde tano, sawa na uwanja mmoja wa mpira wa miguu humomonyoka. Hata hivyo, inachukua miaka 1,000 kuzalisha sentimeta 3 za udongo wa juu ya ardhi.

Kila mwaka zaidi ya tani bilioni 24 za udongo wa juu ya ardhi wa thamani isiyojulikana husombwa na maji au kupeperushwa kote ulimwenguni, kwani ardhi inalimwa kupita kiasi na kulisha mifugo kupindukia na miti na misitu kukatwa.

Ulimwengu utahitaji kuongeza uzalishaji wake wa chakula kwa asilimia kati ya 60 na 70 ili kulisha makadirio ya watu bilioni 9 kufikia mwaka wa 2050 hata kama upanuzi wa sasa wa kilimo unaendelea kutishia misitu na bayoanuai.

Takriban asilimia 75 ya mazao ya matunda na mbegu ulimwenguni hutegemea, angalau kwa kiasi, wachavushaji kama vile nyuki. Wachavushaji huchangia asilimia 35 ya jumla ya uzalishaji wa mazao duniani, na kuchavusha mazao 87 kati ya 115 ya chakula kikuu kote duniani.

**LICHA YA UMUHIMU WAO,** wachavushaji wanadidimia mno, hasa kutokana na mbinu za kilimo, matumizi ya viuatilifu, viumbe vamizi, magonjwa na mabadiliko ya tabianchi.

Kote duniani, angalau watu bilioni 2 hutegemea sekta ya kilimo kwa kipato chao, hasa watu maskini na wa vijijini.

**MIJI**

Miji hukalia chini ya asilimia tatu tu ya ardhi Duniani, lakini ni makazi kwa zaidi ya nusu ya watu duniani.

Miji huchangia asilimia 75 ya matumizi ya rasilimali na nishati duniani na kuzalisha zaidi ya nusu ya taka duniani na angalau asilimia 60 ya uzalishaji wa gesi ya ukaa.

Zaidi ya thuluthi moja ya miji mikubwa, ikijumuisha Barcelona, Bogota, New York na Tokyo, hupata sehemu kubwa ya maji yao ya kunywa ya hali ya juu kutoka kwa misitu iliyohifadhiwa iliyo karibu nao.

Miti katika maeneo ya mijini inaweza kupunguza hewa angani kwa kiasi cha hadi nyuzijoto 5, na hivyo kupunguza mahitaji ya viyoyozi kwa asilimia 25. Miti mijini hutoa manufaa mengi ya kiafya kama vile maji safi. Pia husafisha hewa na kupunguza mafuriko mbali na manufa mengine mengi.

# Mkutano wa Nishati M300 wabeba mazingira Afrika




JANA na leo mataifa yote ya Afrika yataelekeza macho yake ndani ya Tanzania wakati mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu nishati ukiwa umebeba ajenda kuu ya kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya umeme kwa wakazi wote wa bara hili.

Mkutano huo uliopewa jina la Mission 300 (M300) unaongozwa na kaulimbiu inayosema: 'Kuharakisha upatikanaji wa Nishati Afrika', ukiwa na malengo ya kujadili dhana nzima ya upatikanaji wa umeme kwa wote hususan katika nyakati ambazo viongozi wa Afrika wanasisitiza matumizi ya nishati safi na salama.

Tanzania itanufaika na mkutano huo hasa ikizingatiwa kuwa wakuu wa mataifa hayo wataidhinisha Mpango Mahususi wa Nishati wa Afrika, ambao wakuu hao wanakubaliana kufanya mageuzi yatakayosaidia kufikia lengo la upatikanaji wa nishati kwa wote kwa njia za kuaminika, nafuu na endelevu.

Takwimu za nishati kwa Afrika zinaonesha kuwa hadi mwaka 2022 asilimia 83 ya watu milioni 685 walikuwa hawajafikiwa na nishati hiyo. Kwa msingi huo, mkutano huo unadhamiria kuhimiza kuchukuliwa kwa hatua mbalimbali, ikiwemo kuingia makubaliano ili umeme uwafikie watu milioni 300 ifikapo mwaka 2030.

Katika mkutano huo wenye azma ya kuwafikia watu hao milioni 300, nchi 14 zitasaini Mpango Mahususi wa Nishati wa Afrika Awamu ya Kwanza.

Nchi hizo ni Tanzania, Malawi, Chad, Nigeria, Burkina Faso, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Niger, Liberia, Msumbiji, Madagascar, Zambia, Mali, Ivory Coast na Mauritania.

Diplomasia ya kiuchumi ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na nia yake thabiti ya kuibeba ajenda ya nishati safi, ndiyo imefanikisha ujio mkubwa wa viongozi wakuu wan chi za Afrika, ambao wanakutana jijini Dar es Salaam ili kujadili nishati safi na salama.

Akiwa ameibeba ajenda ya nishati salama mkononi mwake, Rais Dk. Samia anatarajiwa kuvunja na kuandika rekodi ya aina yakwe kwa kuwa Rais wa kwanza nchini aliyewahi kupokea idadi kubwa ya wakuu wa nchi 25 kujai kwa pamoja nchini.

Kwetu tunaamini mkutano huo utatoka na majibu ya kina juu ya matatizo ya upatikanaji wa nishati hiyo kwa wakazi wa bara hili na tunawaombea wote heri kubwa, wanapokwenda kujadili na kutatua tatizo la nishati ya umeme barani Afrika.

# Vijana ni muhimu katika utunzaji mazingira

UHARIBIFU wa mazingira ni suala linalopigwa vita na wadau wote wa mazingira duniani kwani licha ya kuharibu mazingira husababisha maafa na uharibifu wa miundombinu.

Yako mazingira mbalimbali yanayosababisha uharibifu wa mazingira kama vile kutotunza vizuri mazingira hao au yale ya asili ikiwamo mafuriko na mabadiliko ya hali ya hewa.

Pamoja na mambo mengine, uwepo wa changamoto kubwa ya uharibifu wa mazingira na utunzaji mazingira na ulinzi kwa vyanzo vya maji ikiwamo maeneo ya misitu nchini.

Mathalani, takwimu za kiserikali zinaonesha kuwa kasi ya uvunaji misitu nchini kwa miaka 10 iliyopita ni kati ya hekta 300,000 hadi 400,000 kwa mwaka.

Katika mkutano wa wakuu wa nchi na wadau wa maendeleo wa Umoja wa Mataifa uliopitisha malengo 17 ya maendeleo endelevu (Development Goals) mwaka 2015 ulitambua kuwa vijana ni rasilimali kubwa na muhimu dunia iliyonayo kwa sasa.

Licha ya utambuzi huo lakini katika sehemu nyingi duniani wamekuwa hawathaminiwi na wakidhaniwa kuwa hawawezi kutimiza baadhi ya malengo.

Serikali na idara zake zinaunga vipi mkono mawazo na juhudi za namna hii? Ni wazi na dhahiri kuwa serikali na wadau wengine wa maendeleo endelevu wanapaswa kuwekeza nguvu kubwa zaidi katika kulinda mazingira nchini, na kwa sasa rasilimali muhimu zaidi ya kutumia ni vijana ambao wameshajiunga katika vikundi au taasisi ndogo ndogo zilizopo nchini kote.

Kwa mfano, serikali isaidie vijana katika kuanzisha vitalu vikubwa vya miti nchini kote katika kila wilaya au jimbo na miti hiyo itolewe kwa bei nafuu au bure kabisa bila ukiritimba wala urasimu kwa jamii ili kuleta hamasa ya upandaji miti. Kwakuwa utunzaji mazingira ni kama falsafa, mpango kama huu ukianzishwa ndani ya miaka mitatu ijayo tutaona jamii ikibadilika na kutambua umuhimu wa ukijani na ukuaji wa kijani nchini.

Lengo la kuleta hamasa ya upandaji wa miti milioni 50 haliwezi kuwa la taasisi moja, au kikundi cha vijana wachache. Ni lengo linalohitaji uungwaji mkono wa serikali, taasisi na sekta binafsi na wadau wote wa maendeleo.

Vijana waungwe mkono na wawezeshwe katika kusaidia kuleta maendeleo katika taifa letu hasa kwenye maswala ya kimazingira na uhamasishaji wa uchumi wa kijani ambao ni ufanyaji wa shughuli za maendeleo kwaajili kupunguza umasikini kwa kuzingatia utunzaji na ulindaji wa mazingira ya asili kwaajili ya kizazi cha leo na cha baadae.

Muhimu zaidi, serikali na wadau binafsi wahakikishe kuwa wanaunga mkono juhudi kama hizi kwa kusaidia pale vijana wanapokwama kwani mipango kama hii kwa vijana siyo ya kibinafsi bali ni ya kijamii na ya kitaifa kwa maendeleo ya sasa na ya baadae.



# VIONGOZI AFRIKA WANAPOIAMULIA AFRIKA YAO

NAMWANDISHI WETU

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amesema baada ya kupata uhuru mwaka 1960, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao.

Dk. Biteko amesema hayo kwenye Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika ‘Mission 300’ unaofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es salaam

Naibu Waziri Mkuu amesema lengo kuu la mkutano huo kuitishwa ni kufikia lengo la kuongeza upatatikanaji wa umeme kwa angalau watu milioni 300 barani Afrika katika miaka mitano ijayo

“Inasikitisha kwamba idadi ya Waafrika ambao hawana umeme inakadiriwa kuwa milioni 571.kutokana na hali hii, Mkutano huu uliitishwa, ukiwa na lengo kubwa lakini linaloweza kufikiwa la kuongeza upatikanaji wa umeme kwa angalau watu milioni 300 barani Afrika katika miaka mitano ijayo

“Kama ilivyobainishwa katika Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), leo Dar es Salaam inayo heshima ya kuwa mwenyeji wa wajumbe kutoka Afrika na kwingineko, wakihudhuria Mkutano huu muhimu unaolenga kuimarisha azma ya Afrika ya kuipatia bara hili nishati.

“Baada ya kupata Uhuru mwaka 1960, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao. Tanzania ilikuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 21 pekee wakati wa Uhuru, kwa sasa nchi ina uwezo wa kuzalisha megawati 3,160.

“Pamoja na mafanikio makubwa ya kuzalisha umeme barani Afrika, takriban Waafrika milioni 571 bado hawana huduma ya umeme. Mkutano huu umeitishwa rasmi kwa lengo la kujadili namna ya kuongeza upatikanaji wa umeme kwa watu milioni 300 barani Afrika katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

“Natoa shukrani za dhati kwa waandaaji wenza wa Mkutano huu ikiwemo: Benki ya Dunia; Benki ya Maendeleo ya Afrika; Rockefeller Foundation; Sustainable Energy for All (SEforALL), na The Global Energy Alliance for People and Planet (GEAPP) kwa ushirikiano uliowezesha kufanyika kwa Mkutano huu.

“Uwepo wenu, mawazo na utaalamu wenu ndiyo vitakavyofanikisha Mkutano huu. Natarajia majadiliano yenye tija na tushirikiane katika kuunda mustakabali wa nishati barani Afrika.

“Natarajia mkutano huu utakuwa ni hatua muhimu katika kufanikisha lengo letu la upatikanaji wa umeme kwa wote.

“Katika mkutano huu, Mawaziri wa Nishati, Viongozi wa Taasisi za Kimataifa za Kifedha, Wataalam na Wadau wa Mashirika ya Kiraia, watapata fursa ya kujadili na kukubaliana malengo, vipaumbele vya sera, suluhisho, na ahadi za jinsi ya kutekeleza Mpango wa Mission 300.



“Maazimio ya Nishati ya Kitaifa yaliyotayarishwa na nchi 14 zitakazokuwa za majaribio yatatoa mfumo wa utekelezaji wa hatua zilizoratibiwa ili kufungua uwekezaji zaidi kutoka kwa serikali, wabia wa maendeleo, mashirika ya misaada na sekta binafsi katika kufanikisha malengo ya upatikanaji wa nishati.

“Kupitia uhamasishaji wa rasilimali na utaalamu katika kuharakisha juhudi za kupeleka umeme barani Afrika, Mission 300 itaonyesha dhamira yetu ya pamoja katika kufanikisha upatikanaji wa nishati safi kwa wote, kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na kuboresha maisha ya watu.

“Tanzania inachukulia mkutano huu kama kichocheo cha utekelezaji wa Sera yake ya Taifa ya Nishati inayolenga kuendeleza nishati endelevu, uhifadhi na ufanisi. Sera hiyo pia inalenga kuongeza upatikanaji wa huduma za kisasa za nishati na kuongeza mchango wa nishati mbadala katika mchanganyiko wa uzalishaji ili kuimarisha upatikanaji, uhakika na usalama wa nishati.

“Ifikapo mwisho wa mwaka 2025, uwezo wa Tanzania kuzalisha umeme utaongezeka hadi megawati 4,000. Nishati yetu inatoka kwenye vyanzo safi na mbadala vinavyonufaisha wakazi wa vijijini na mijini, huku miundombinu ya umeme ikifikia vijiji vyote 12,318 nchini.

“Vile vile, Tanzania inamarisha muunganiko wa Afrika kwani ina miundombinu ya umeme inayounganisha nchi za Kenya, Burundi, Rwanda, na Uganda, huku miundombinu ya kuunganisha Zambia ikiwa inaendelea.

“Pamoja na maendeleo ya nishati tunayojivunia, bado nchi inahitaji uwekezaji zaidi katika sekta ya nishati. Tuna matarajio ya kukuza shughuli za kiuchumi hususan katika sekta za viwanda, madini, na huduma za ukarimu jambo ambalo linahitaji uwekezaji wa kimkakati zaidi katika sekta ya nishati.

“Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele katika kukuza upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani Afrika. Jitihada hizi zimeungwa mkono na mkakati wa kitaifa na yamejumuishwa katika Azimio litakalotiwa saini, huku tukitoa wito wa ahadi na ushirikiano zaidi katika kuboresha upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani mwetu.

“Miongoni mwa mambo mengine yatakayofanyika katika mkutano huu, tutashirikiana uzoefu; kupata ahadi muhimu za kisiasa; kutumia ushirikiano ili kufungua uwekezaji wa sekta binafsi; kuanzisha ushirikiano wa kufadhili miundombinu ya nishati; na kukubaliana mfumo wa ufuatiliaji, ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kiashiria cha Ufuatiliaji wa Maazimio ili kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa kwenye Mkutano huu.

“Ni matarajio yangu kwamba, mamlaka zinazohusika za nishati katika kila nchi ya majaribio zitajitahidi kuhakikisha maazimio ya nishati yanafanikishwa kupitia malengo na mipango ya hatua zinazolenga kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme, matumizi ya nishati safi ya kupikia, nishati mbadala na mchango wa mtaji wa sekta binafsi katika kufanikisha upatikanaji wa nishati.

“Sasa ni wakati wa kufungua uwezo wa nishati wa bara la Afrika na kukabiliana na pengo la nishati. Tuitumie fursa ya Mkutano huu kuhitimisha Maazimio yanayoendana na matarajio yetu ya nishati na kuimarisha ushirikiano unaohitajika kuyatekeleza.

Naye Rais wa Benki ya Dunia (WB), Ajay Banga katika mkutano huo, aliyasema haya;

“Tunaweza kubadilisha sura ya Afrika kwa kuwa na juhudi za pamoja za kuunganisha rasilimali zilizopo kuhakikisha nishati ya umeme inawafikia wananchi wengi zaidi Afrika ifikapo 2030.”

Rais wa Benki ya Maendele ya Afrika (AfDB), Dk Akinumwi Adesina alisema: “Tanzania imekua mfano wa kuigwa kwa kufanya vizuri katika uwekezaji wa miundombinu ya umeme kwa kuwafikishia nishati ya umeme wananchi katika vijijini vyote 12,318.

“Nawahakikishia kuwa lengo la kuwafikishia umeme watu milioni 300 Afrika linakwenda kufanikiwa, tunahitaji uwazi na uwajibikaji katika kufikisha lengo hili.

“Mkutano huu una lengo la kuifungua Afrika kwenye eneo la nishati ya umeme, kuhakikisha wananchi katika za Afrika wanaunganishwa na umeme.”

# Mambo 10 ya kushangaza Hifadhi ya Serengeti - 2

NA MWANDISHI WETU

HIFADHI ya Taifa ya Serengeti ni mojawapo ya hifadhi za wanyamapori zinazothaminiwa zaidi duniani, maarufu kwa viumbe hai na uzuri wa asili.

Hifadhi hii ya thamani kwenye ardhi ya Tanzania inaficha siri nyingi na ukweli wa kuvutia unaosubiri kugunduliwa na msafiri na mpenda asili. Tunakaribia kuzama ndani ya kina cha kile kinachoifanya Serengeti kuwa ya kipekee sana kwa mambo kumi ya kushangaza ambayo yanatoa taswira ya uchangamano na maajabu ya hifadhi hii ya ikolojia.

Endelea…

**4. Mahali kwa Viumbe vilivyo Hatarini Kutoweka**

Serengeti sio tu nyumbani kwa idadi kubwa ya megafauna ya haiba, lakini pia mahali patakatifu kwa spishi zilizo hatarini. Miongoni mwa wakazi wake mashuhuri ni faru weusi na mbwa mwitu wa Kiafrika, wote wameainishwa kuwa hatarini na Muungano wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Mazingira (IUCN).

Hifadhi hiyo ni mojawapo ya ngome za mwisho zilizosalia kwa faru weusi, huku juhudi za makusudi zikilenga kupambana na ujangili na kuhifadhi makazi ili kuongeza idadi yao.

Jambo lisilojulikana sana ni umuhimu wa Serengeti kwa uhifadhi wa duma. Hifadhi hii ina mojawapo ya idadi kubwa zaidi ya paka hawa wenye kasi, ikitoa nafasi adimu ya kuwaona katika makazi yao ya asili, ambapo wanahitaji maeneo makubwa kuwinda na kuishi.

Huku idadi yao ikipungua mahali pengine kutokana na upotevu wa makazi na migogoro ya binadamu na wanyamapori, Serengeti bado ni muhimu kwa mustakabali wao.

**5. Nyumbani kwa Ol Doinyo Lengai**

Iliyowekwa karibu na mipaka ya Serengeti ni Ol Doinyo Lengai ya ajabu, volkano pekee inayoendelea Tanzania. Jina linalomaanisha 'Mlima wa Mungu' katika lugha ya Kimaasai, volcano hii ina nafasi ya pekee katika mioyo na mila za jamii ya kimasai.

Ol Doinyo Lengai ni ya kipekee kati ya volkeno za dunia kutokana na lava yake ya nadra ya kaboni, ambayo ni baridi zaidi kuliko lava nyingi na ina rangi nyeusi ya kipekee wakati wa mchana na muundo wa kiowevu ambao karibu unafanana na mto wa mafuta unapolipuka.

Athari za Ol Doinyo Lengai kwenye Serengeti ni kubwa. Majivu yake hurutubisha tambarare zinazoizunguka, na imesaidia kutengeneza mazingira kwa muda mrefu kupitia milipuko ya mara kwa mara.

Shughuli ya volcano inachangia udumishaji wa viumbe hai wa nyanda za juu na mabadiliko ya kijiolojia ya eneo hilo. Kwa wanaotafuta msisimko na wapendajiolojia, fursa ya kushuhudia kilele cha volkano au hata kuipanda ni kipengele cha kuvutia cha mazingira ya hifadhi hiyo.

**6. Pepo ya Mtazamaji Ndege**

Serengeti ambayo mara nyingi hufunikwa na mamalia maarufu wa nchi kavu, ni paradiso kwa watazamaji wa ndege. Kwa kujivunia zaidi ya spishi 500 za ndege, mbuga hiyo hutoa makazi kwa anuwai ya viumbe vya ndege, kutia ndani ndege wakubwa zaidi ulimwenguni, mbuni, na ndege mzito zaidi anayeruka, Kori bustard.

Aina mbalimbali ni kutoka kwa roller yenye matiti ya lilac hadi tai mkuu wa kijeshi. Mandhari mbalimbali ya bustani - ambayo ni pamoja na savanna, vinamasi, misitu, na kopjes - inasaidia idadi ya ndege tofauti kwa usawa.

Kinachoifanya Serengeti kuwa ya pekee kwa wanaopenda ndege ni idadi ya spishi ambazo hazipatikani kwingineko duniani. Ndege kama vile spurfowl mwenye matiti ya kijivu, mfumaji mwenye mkia wa Rufous, na barbeti ya Usambiro ni hazina kwa orodha ya maisha ya watazamaji ndege.

Zaidi ya hayo, mbuga hiyo ni tovuti muhimu kwa ndege wanaohama, ambao hutumia Serengeti kama kisimamo katika safari zao ndefu, na kuongeza aina mbalimbali za msimu kwa uzoefu wa kuangalia ndege.

**7. Mchoro Mzuri wa Tamaduni za Kikabila**

Zaidi ya wanyamapori wake, Serengeti pia ina utajiri wa urithi wa kitamaduni. Hifadhi hiyo na maeneo yanayoizunguka ni makazi ya takriban makabila 120 tofauti, huku Wamasai wakiwa ndio wameenea zaidi.

Wamasai ni watu wasiohamahama wanaojulikana kwa mila na mavazi yao tofauti, na mtindo wao wa maisha umefungamana kwa karibu na ardhi hii kwa karne nyingi.

Wanaishi pamoja na wanyamapori, ng'ombe wao wakichunga kwenye tambarare sawa na wanyama wa porini, katika uwiano mpole ambao umekabiliana na changamoto zake na kuanza kwa jitihada za kisasa za uhifadhi.

Watalii wengi hufurahia fursa ya kujifunza na kujihusisha na mila za kale za Wamasai, ambazo ni pamoja na ibada za kupita, ngoma, na kusimulia hadithi. Kutembelea kijiji cha kimapokeo cha Wamasai au 'boma' kunaweza kutoa uelewa wa kina wa muktadha wa kibinadamu ambao unaingiliana na historia ya asili ya hifadhi.

Nafasi ya kushuhudia kuwepo kwa pamoja kwa binadamu na wanyama, wakati mwingine kwa maelewano na wakati mwingine katika migogoro, inaongeza safu chungu kwenye hadithi ya Serengeti.

**8. Safari za Baluni ya Air Moto**

Hebu wazia ukielea juu ya mandhari ambayo haijafugwa ya Serengeti, ukitazama macheo ya jua yakipaka rangi tambarare kwa rangi ya dhahabu. Safari za puto za hewa moto hutoa mtazamo huu wa kipekee na zimekuwa njia inayotafutwa ya kufurahia bustani.

Ukiwa mahali panapoonekana angani, ukimya tulivu hukufunika unapoelea juu ya makundi ya wanyama na kushuhudia ukubwa wa ajabu wa mbuga hiyo kutoka juu. Ni tofauti ya amani kwa viendeshi vya kawaida vya mchezo na hutoa fursa ya kutazama isiyo na kifani.

Matukio haya ya angani sio tu ya kuvutia na mandhari yake ya ajabu lakini pia huchangia mazoea ya utalii ambayo ni rafiki kwa mazingira.

Puto huteleza kwenye mbuga bila usumbufu mdogo kwa wanyamapori, na waendeshaji hudumisha dhamira thabiti ya uhifadhi na ushirikishwaji wa jamii. Wageni wengi wanaona kuwa safari ya puto sio tu kuwa kivutio cha wakati wao Serengeti lakini pia zoezi la utalii wa kuwajibika.

**9. Nafasi katika Utafiti na Elimu**

